



*(University of Choice)*

**MASINDE MULIRO UNIVERSITY OF  
SCIENCE AND TECHNOLOGY  
(MMUST)**

**MAIN  
UNIVERSITY EXAMINATIONS  
2023/2024 ACADEMIC YEAR**

**FOURTH YEAR FIRST SEMESTER EXAMINATIONS**

**FOR THE DEGREE  
OF  
BACHELOR OF EDUCATION ARTS**

**COURSE CODE: KIS 404**

**COURSE TITLE: EDITORIAL METHODS IN KISWAHILI**

**DATE: Monday 11<sup>th</sup> December, 2023      TIME: 12.00-2.00PM**

---

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA**

**Jibu swali la Kwanza (1) na mengine Mawili (2)**

**TIME: 2 Hours**

MMUST observes ZERO tolerance to examination cheating

This Paper Consists of 2 Printed Pages. Please Turn Over.

1. a) 'Mwandishi, mhariri na mchapishaji ni wadau wanaotegemeana katika utendakazi wao' Jadili kauli hii kwa kutumia mifano maridhawa.

**(Alama 20)**

b) Hariri makala yaliyoambatishwa kwa kutumia alama madhubuti za uhariri

**(Alama 10)**

2. Jadili aina zozote **tano** za sheria zinazozingatiwa katika uchapishaji

**(Alama 20)**

3. Jadili njia ambazo zinatumiwa katika uuzaji na usambazaji wa kitabu baada ya kuchapishwa

**(Alama 20)**

4. Kwa kutumia mifano mwafaka, fafania mambo muhimu ya kuzingatiwa katika aina zifuatazo za uhariri:

i. Uhariri wa vielelezo

ii. Uhariri wa picha

**(Alama 20)**

5. Eleza historia na maendeleo ya uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili katika Afrika Mashariki kuanzia enzi za wamishenari hadi wakati wa sasa.

**(Alama 20)**

6. Kwa mifano mwafaka, eleza dhima kuu anazotekeleza mhariri wa vitabu vya kiada katika shirika la uchapishaji.

**(Alama 20)**

## **Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki**

HISTORIA ya Kiswahili inapambanua ukubwa wake pamoja na mchango wake katika maendeleo ya mataifa ya Afrika Mashariki na Kati. Kiswahili kimekuwa ni miongoni mwa nyenzo muhimu katika kuimarisha muungano wa Afrika Mashariki tangu wakati wa ukoloni mpaka sasa. Kwa muda mrefu lugha ya mawasiliano ya Afrika Mashariki na nchi za maziwa makuu imekuwa ni Kiswahili na kimekuwa kikiimarishwa na uwapo wa jumuiya ya Afrika Mashariki.

Lichaya kuimarika kwa matumizi ya Kiswahili miongoni mwa nchi za jumuiya, kunapaswa kuchukuliwa hatua madhubuti zaidi kwa ajili ya kuhakikisha lugha ya Kiswahili inakuzwa na kuendelezwa miongoni mwa nchi ambazo bado hazijaimarika katika matumizi ya Kiswahili. Miongoni mwa juhudi na mikakati hiyo ilikuwa ni kuundwa kwa Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki chini ya jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na makao yake makuu yakapelekwa visiwani Zanzibar.

Kutokea hapo shughuli nyingi za ukuzaji wa Kiswahili, tafiti, uandaaji wa makongamano makubwa na semina mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki na kati zimekuwa zikisimamiwa na kamisheni hii na hakuna ubishi kwamba kamisheni hii imesaidia pakubwa katika kuimarisha umoja na mshikamano kupitia lugha ya Kiswahili katika jumuiya.

Baadhi ya shughuli za kamisheni ya Kiswahili ni kama vile

Makongamano, huwa ni matukio muhimu ya kuleta Utangamano miongoni mwa wakereketwa, wataalamu na wanafunzi wa Kiswahili ambayo huandaliwa na Kakama kwa ajili ya mafunzo mbalimbali. Kakama imekuwa na desturi ya kuwakusanya pamoja kwa nia ya kujadili masuala mbalimbali kuhusu Kiswahili pamoja na mustakabali wake Afrika Mashariki kwa gharama kubwa kutoka kwa nchi wanachama na kucheleweshwa kwa fedha hizi kunaweza kuathiri makongamano.

tafiti, Kamisheni hii ina Wataalamu na wanaisimu mbalimbali ambao wapo kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali kuhusu lugha, utamaduni, fasihi ya Kiswahili na uhusiano wake na lugha nyingine ndani na nje ya mipaka ya Afrika Mashariki ambapo huhitaji fedha nyingi ili kukidhi gharama mbalimbali. Kitendo cha bunge kuchelewa kupitisha bajeti kinachelewesha kama si kukosesha kabisa kamisheni ya Kiswahili kufanya tafiti ambazo ni



muhimu katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili. Ipo haja ya wabunge hawa kutimiziwa mahitaji yao kwa wakati ili shughuli muhimu kama hizi zisikwame au kusuasua.

machapisho, kakuwa ni taasisi inayofanya shughuli nyingi za uandishi na utafiti, kila wakati machapisho mbalimbali huchapishwa kwa gharama. Kamisheni ya Kiswahili inaweza kushindwa kumudu gharama za uchapishaji wa taarifa na tafiti mbalimbali kwa bajeti kuchelewa na hivyo kuzorotesha shughuli za uenezaji na ukuzaji wa Kiswahili sehemu mbalimbali za Afrika na nje ya Afrika.

shughuli za ukuzaji na uenezaji wa kiswahili hazipaswi kurudi nyuma kamwe, tayari tupo kwenye mstari ulionyooka na hatupaswi kusimama. Nchi wanachama ziunganishe nguvu kwa mara nyingine ili kuwe na fedha za kutosha kwa ajili ya miradi mingine pamoja na Kakama kwani ndio nguzo muhimu ya kiswahili inayoimamisha jumuiya ya Waswahili Afrika

